

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI

11 MEI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI – TAREHE 11 MEI, 2017

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

185. MHESHIMIWA AMINA SALEH MOLLEL
(VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Masuala ya watu wenye ulemavu kwa kiasi kikubwa yanazungumzwa na kushughulikiwa katika maeneo ya Mijini na kusahau maeneo ya pembezoni ambapo kuna watu wa jamii hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhusu watu wenye ulemavu waishio Vijijini ambapo matatizo yao ni mengi na makubwa kulingana na jamii inayowazunguka.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

186. MHESHIMIWA SALOME WYCLIFFE MAKAMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais aliyoitoa wakati wa kampeni kwa Wananchi wa Jimbo la Kahama Mjini ya kujenga kwa kiwango cha lami kilomita 10 za barabara za Mitaa ya Mji wa Kahama.

187. MHESHIMIWA RICHARD PHILIP MBOGO (NSIMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Vifo vya Mama na Mtoto vinachangiwa na huduma hafifu ikiwemo ukosefu wa usafiri hasa gari la kubebea wagonjwa (*ambulance*).


Je, ni lini Serikali itatoa gari la wagonjwa kwa Jimbo la Nsimbo.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

188. MHESHIMIWA VEDASTO EDGAR NGOMBALE (KILWA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Maeneo mengi ya Jimbo la Kilwa Kaskazini bado hayajapata huduma ya mawasiliano ya simu kama vile Kata za Kibata, Kinyumbi, Kandawale na Vijiji vya Nandete na Mkarango:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hii katika maeneo hayo.



WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

189. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Vijiji 48 vya Jimbo la Same Magharibi vyenye zaidi ya Kaya 2943 havijapatiwa umeme wa REA japokuwa vina mahitaji makubwa ya umeme:-

Je, ni ipi ratiba ya kuwasambazia umeme Wananchi hawa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(Majadiliano yanaendelea)



**DODOMA
11 MEI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**